KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

# Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Tanzania



# Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Tanzania

*Kitini hiki cha Utatuzi wa Migogoro ya ArdhiTanzania kimeandaliwa na PELUM Tanzania kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo la Msaada la Watu wa Marekani (USAID). PELUM Tanzania inawajibika kwa maudhui yaliyomo ndani ya kitini hiki na maudhui hayo hayawakilishi msimamo wa USAID au Serikali ya Marekani.*

# Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Tanzania

© PELUM Tanzania 2015

ISBN 978-9987-8956-8-7

Mchora Katuni: Godwin J. Chipenya

**Kwa mawasiliano zaidi:**
Mratibu,
PELU M Tanzania
S.L.P 390, Morogoro-Tanzania
Simu/Nukushi: +255 23 2613677
Barua pepe: info@pelumtanzania.org
Tovuti: www.pelumtanzania.org

## YALIYOMO


**Shukrani** 1

**1.0 Utangulizi** 2

**2.0 Maana ya Migogoro ya Ardhi** 3
- 2.1 Aina ya Migogoro ya Ardhi 3
- 2.2 Vyanzo na Viashiria vya Migogoro ya Ardhi 3
- 2.3 Madhara Yatokanayo na Migogoro ya Ardhi 4
- 2.4 Mbinu na Njia za Kuzuia Migogoro ya Ardhi 5

**3.0 Njia za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Tanzania** 7
- i. Njia ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Isiyo Rasmi 7
- ii. Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Iliyo Rasmi 7

**4.0 Vyombo vya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi** 9
- 4.1 Baraza la Ardhi la Kijiji 9
- 4.2 Baraza la Kata 11
- 4.3 Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya 14
- 4.4 Mahakama Kuu 16
- 4.5 Mahakama ya Rufaa 17

**5.0 Changamoto** 19

**6.0 Hitimisho** 20

## SHUKRANI

Kitini cha Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi kimeandaliwa na shirika la PELUM Tanzania kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Msaada la Watu wa Marekani (USAID) kupitia Mradi wa Ushiriki wa wananchi katika kusimamia sekta ya Kilimo (Citizen Engaging in Government Oversight) unaolenga kuhusisha ushiriki wa wananchi kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali pamoja na uwajibikaji wa serikali kwa ujumla katika masuala ya ardhi.
Kitini hiki kimeandaliwa mahususi kwa jamii ya wazalishaji wadogo na wanaopenda kujisomea. Lengo kuu la kitini hiki cha utatuzi wa migogoro ya ardhi ni kukuza ufahamu na uelewa wa jamii juu ya mfumo wa vyombo vya utoaji maamuzi juu ya ardhi na kuwawezesha wazalishaji wadogo waishio vijijini kushiriki katika masuala ya ardhi ili waweze kudai, kutetea na kulinda haki zao za ardhi kwa manufaa yao na kizazi kijacho. Kitini hiki kinaweza kuwa nyenzo muhimu sana kwa wasomaji na wazalishaji wadogo kwa kuwa kitini hiki kinajumuisha mifumo mbalimbali ya utatuzi wa migogoro ya ardhi, ambayo inawapa wananchi uhuru wa kuchagua mfumo gani ni sahihi kwa wao kuweza kufikia muafaka katika kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo yao husika.

PELUM Tanzania inapenda kutoa shukrani za dhati kwa timu ya wafanyakazi wake wote kwa kuandika Kitini hiki na kukisadifu kwa kina. Pia inapenda kuwashukuru Wanachama wa PELUM Tanzania; Tanzania Grass Roots Oriented Development (TAGRODE, Uluguru Mountains Agricultural Development Project (UMADEP) na Institut Africain pour le Développement Economique et Social (INADES Information Tanzania) na Wadau mbalimbali ambao walisoma kitini hiki na kutoa maoni yao katika kuboresha kitini.

Pia, shukrani za pekee ziende kwa Asasi za Kiraia; Lawyers' Environmental Action Team (LEAT), Naramatisho Pastoralists Society (NAPASO), HAKIARDHI, na Pamoja Twajenga. Aidha, shukrani zetu za dhati ziende kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Mendeleo ya Makazi, Halmashauri zote za Kilolo, Mufindi, Bahi, Kongwa, Mvomero na Morogoro Vijijini, bila kusahau wataalamu wa lugha ya Kiswahili, Baraza a Kiswahili la Taifa (BAKITA) kwa mchango wao wa usanifu wa lugha katika kitini hiki. Mwisho kabisa na kwa namna ya pekee PELUM Tanzania inapenda kulishukuru Shirika la Misaada ya Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID) kwa kutoa ufadhili kwa mradi wa Ushiriki wa wananchi katika kusimamia sekta ya Kilimo unaotekelezwa na PELUM Tanzania ambao umefanikisha kuandikwa na kuchapishwa kwa kitini hiki.

# 1.0 UTANGULIZI

Ardhi ina umuhimu mkubwa katika maisha ya binadamu. Ardhi ni moja ya rasilimali za msingi katika Uhai na Maendeleo ya Binadamu, Wanyama, Mimea na Viumbe vyote. Ongezeko la watu, maendeleo ya kiteknolojia, kiuchumi na kijamii, vimepelekea uhitaji mkubwa wa ardhi kwa makundi mbalimbali hali ambayo husababisha ardhi kupanda thamani na wakati mwingine husababisha kuibuka migogoro baina ya watumiaji wa ardhi.

Ugawaji, Umilikaji wa ardhi na maamuzi yanayofanyika na mamlaka mbalimbali kuhusiana na ardhi wakati mwingine husababisha migogoro ya ardhi ya hapa na pale. Ili kuhakikisha haki inatendeka na watu wote wanapata haki katika kupata na kumiliki ardhi, migogoro hiyo yote haina budi kusuluhishwa na kutatuliwa kwa mujibu wa taratibu za asili na za kisheria ambazo zipo. Kitini hiki kinachambua vyanzo vya migogoro, athari zake, pamoja na mbinu mbalimbali zinazotumika kuitatua migogoro hiyo kwa mujibu wa mfumo usio rasmi na ule ulio rasmi yaani unaofuata sheria za nchi.

## 1.1 MALENGO YA KITINI

i. Kitini hiki kimekusudia kuchambua na kujadili mbinu mbalimbali za usuluhishi wa migogoro ya ardhi Tanzania, zinazoweza kutumiwa na jamii (hasa wazalishaji wadogowadogo) katika kutatua, kuzuia, na kupunguza migogoro ya ardhi katika maeneo yao.

ii. Kitini hiki kimelenga kuongezea uelewa, maarifa na ujuzi hasa kwa viongozi na wajumbe wa Mabaraza na Mahakama za ardhi wakati wa kuendesha mashauri yanayo husiana na ardhi.

iii. Kitini hiki kitakuwa rejea muhimu sana kwa jamii za vijijini na Mijini pale wanapokumbana na suala zima la kutatua migogoro ya ardhi.

iv. Kijitabu hiki kitasaidia sana kukuza uelewa kwa wananchi kuhusu haki zao kwa mujibu wa sheria wakati wote wa mwenendo wa mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi.

## 2.0 MAANA YA MIGOGORO YA ARDHI

Migogoro ya ardhi ni hali ya kutofautiana kimaslai baina ya pande mbili au zaidi juu ya umiliki, matumizi, upatikanaji na usimamizi wa ardhi na rasilimali zilizopo katika ardhi.

### 2.1 AINA YA MIGOGORO YA ARDHI

Baadhi ya migogoro inayofahamika ni kama ilivyoainishwa hapa chini:

a. Wakulima na wafugaji kugombania rasilimali adimu kama vile maji na malisho.
b. Kijiji dhidi ya kijiji wakigombea mipaka.
c. Halmashauri ya kijiji kupitisha maamuzi ya ugawaji ama utwaaji wa ardhi ya kijiji bila ya kushirikisha wananchi.
d. Taasisi za kiserikali, kidini na kibinafsi dhidi ya wanavijiji hasa pale taasisi hizi zinapotanua maeneo yao hadi kwenye maeneo ya kijiji.
e. Mamlaka za hifadhi dhidi ya wanavijiji kutokana na kupanuka kwa hifadhi hadi kwenye maeneo ya wanavijiji bila mawasiliano wala kufuata taratibu. Vile vile baadhi ya wanavijiji kuvamia maeneo ya hifadhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji.
f. Wachimbaji wadogo wa madini dhidi ya wachimbaji wakubwa. Hii ni kutokana na baadhi ya wachimbaji wakubwa kuingia maeneo ya wachimbaji wadogo bila kufuata taratibu zinazotakiwa zikiwemo kulipa fidia inayostahili vilevile wachimbaji wadogo kuvamia wachimbaji wakubwa.
g. Migogoro baina ya mtu na mtu.
h. Wananchi na wawekezaji wakubwa kwenye ardhi

### 2.2 VYANZO NA VIASHIRIA VYA MIGOGORO YA ARDHI

Migogoro ya ardhi kwa Tanzania inasababishwa na mambo kadha wa kadha. Kitini hiki kimejaribu kuainisha baadhi ya vyanzo na viashiria vya migogoro ya ardhi ili kumsaidia mwananchi kutambua ni kwa namna gani migogoro ya ardhi hutokea na zipi ni dalili za migogoro ya ardhi kuibuka. Hii itasaidia sana kwa mwananchi kuona chanzo au dalili za kuibuka kwa mgogoro wa ardhi, na kuweza kuchukua hatua stahiki kwa wakati, kwa kuziarifu mamlaka husika kama suala lenyewe limo ndani ya uwezo wa chombo hicho. Zifuatazo ni baadhi tu ya vyanzo na viashiria vinavyoweza kusababisha migogoro ya ardhi kuibuka katika

eneo:

a. Sheria za ardhi kutofahamika vizuri miongoni mwa wananchi na viongozi na hivyo kutofahamu haki na wajibu wao juu ya ardhi
b. Ukiukwaji wa Sheria zinazo simamia ardhi kwa baadhi ya watendaji kwa mfano, kugawa eneo moja kwa watumiaji zaidi ya mmoja.
c. Kuendelea kupanuka kwa Miji na kumeza maeneo ya vijiji.
d. Ongezeko kubwa la wawekezaji katika ardhi kunafanya wananchi wengi kuondolewa kwenye maeneo yao yenye rutuba pasipo kufuata utaratibu wa kuwalipa fidia stahiki, ya haki, na ya wakati.
e. Upanuzi wa barabara na miundo mbinu mingine, husababisha wananchi wengi kuvunjiwa maeneo yao ya makazi.
f. Mitazamo hasi juu ya kundi la watu fulani na utaratibu wao wa kuzalisha mali, mfano wafugaji na wakulima.
g. Uhaba wa rasilimali ardhi katika eneo fulani huweza kuibua migogoro ya ardhi, Mfano kupungua kwa nyanda za malisho kwa upande wa wafugaji, huwalazimisha kuingiza mifugo yao kwenye maeneo yaliyo tengwa kwa ajili ya kilimo.
h. Wananchi kutoshirikishwa na kukosekana kwa uwazi juu ya usimamizi na maamuzi katika masuala yanayohusu ardhi.
i. Kukosekana kwa mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi katika eneo husika.

## 2.3 MADHARA YATOKANAYO NA MIGOGORO YA ARDHI

Siku zote zao la mgogoro wa aina yoyote ni madhara ya aina fulani. Kitini hiki kimejaribu kuainisha baadhi tu ya madhara yanayotokana na migogoro ya ardhi, ili msomaji apate kutambua matatizo yanayotokea pindi migogoro ya ardhi inaposhindwa kutatuliwa. Madhara hayo yanaweza kuwa ya kijamii, kiuchumi, na pengine hata ya kisiasa. Kilosa, Kiteto na Loliondo ni sehemu tu ya mifano kwa Tanzania, inayoonesha ni jinsi gani migogoro ya ardhi ilivyo waathiri wazalishaji wadogowadogo (wakulima na wafugaji). Yafuatayo ni baadhi tu ya madhara yanayoweza kusababishwa na migogoro ya ardhi:

a. Uhasama, chuki na mgawanyiko miongoni mwa jamii na kukuza tofauti baina ya watu au kikundi cha watu walio ndani ya migogoro ya ardhi.
b. Kusababisha majeraha na mara nyingine kupoteza uhai wa binadamu na wanyama pia.

c. Kupungua kwa uzalishaji mali na mazao ya chakula kutokana na kupoteza muda mwingi kwenye kutatua migogoro ya ardhi.
d. Kupotea kwa amani katika jamii husika.
e. Kudumaza maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, kwa kuwa rasilimali kubwa inatumika katika kutatua migogoro ya ardhi na kuacha sekta zingine zikidumaa.
f. Kukosekana kwa huduma za kijamii kama vile kufungwa kwa zahanati,shule,barabara na n.k




## 2.4 MBINU NA NJIA ZA KUZUIA MIGOGORO YA ARDHI

Zifuatazo ni baadhi ya mbinu au njia ambazo mwananchi hana budi kuzisoma na kuzielewa vyema, ili aweze kuziepuka na kuzuia kuibuka kwa migogoro ya ardhi. Kama tujuavyo usemi huu wa Kiswahili usemao **"Kinga ni bora kuliko Tiba"**, msemo huu unatukumbusha wanajamii hasa sisi wazalishaji wadogo tusisubiri mpaka migogoro ya ardhi iibuke au ifikie hatua ya kuleta madhara ndiyo tuanze kuitatua, bali tuchukue hatua mapema zaidi kabla madhara hayajatokea.

Hizi ni baadhi ya njia na mbinu mbalimbali zinazoweza kusaidia kuzuia na kuepuka migogoro ya ardhi Tanzania.

a. Kujenga uwezo wa kisheria kwa vyombo/mamlaka zinazohusika na usimamizi wa ardhi ili viweze kusimamia kwa misingi ya haki.
b. Kuwezesha uundwaji na utekelezaji wa mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi vijijini.
c. Watendaji wenye mamlaka ya juu ardhi kufuata sheria na taratibu katika kusimamia ardhi ili kuepusha migogoro ya ardhi isiyo ya lazima.
d. Kuepuka dalili zozote zinazoashiria mgogoro ya ardhi.
e. Sheria zote zinazosimamia ardhi zifundishwe kwa wananchi wote ili waweze kujua haki zao na wajibu wa msingi juu ya ardhi.
f. Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kila eneo litambuliwe kwa kupimwa.
g. Wananchi washirikishwe katika kutoa maamuzi yanayohusiana na mustakabali wa ardhi yao.
h. Kuhimiza ushiriki, ushirikishwaji na uwazi katika usimamizi na maamuzi ya ardhi vijijini.

## 3.0 NJIA ZA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI TANZANIA

Kuna njia kuu mbili za utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini Tanzania, moja ni utatuzi wa migogoro kwa njia **isiyo rasmi** na pili ni njia **iliyo rasmi**.

***i. Njia ya utatuzi wa migogoro ya ardhi isiyo rasmi***

Migogoro ya ardhi Tanzania haikuanza leo wala jana au wakati wowote wageni kutoka nje walipoanza kuingia, iliaanza zamani sana. Hata historia ya mfumo wa kumiliki ardhi Tanzania inaonesha, uwepo wa migogoro hiyo hata kabla ya ujio wa wageni (wakoloni). Wazee wetu wa zamani walikuwa na migogoro ya ardhi mingi tu, kati ya Koo na koo, utawala na utawala kugombea himaya au maeneo yao ya uzalishaji. Hata hivyo wazee hawa walikuwa na utaratibu na mfumo wao wa kutatua migogoro hiyo pale ilipoibuka. Wazee wa Kimila, Machifu, Wakuu wa Koo na Wazee wanao heshimika katika eneo husika, ndio walikuwa wasuluhishi wa migogoro ya ardhi kwa kuzingatia mila zao.

Mfumo huu huitwa mfumo usiyo rasmi kwa sababu haufuati taratibu za kisheria kama vilivyo vyombo vinginevyo mfano; mahakama na mabaraza ya ardhi. Mfumo huu pamoja na kutotambulika kisheria ni mfumo ambao mpaka hivi leo kuna baadhi ya maeneo unatumiwa na jamii husika katika kutatua migogoro ya ardhi na umekuwa na utendaji mzuri kabisa. Mfano Kabila la Wamaasai limekuwa likitumia wazee wanaoitwa “Laigwanan”katika kusuluhisha migogoro yote ya kijamii likiwemo suala la ardhi.

Kuna manufaa gani kutumia mfumo huu?

a. Mfumo huu hauna gharama zozote za kifedha.
b. Suluhu hufanyika karibu kabisa na jamii husika. mfano kijijini.
c. Lugha inayotumika ni ya wenyeji husika, hakuna tatizo la lugha.
d. Muafaka hufikiwa pasipo kujengeana chuki.
e. Mfumo huu pia hauna ushawishi wa rushwa.
f. Wasuluhishi wanaelewa mila na desturi za wenyeji.

***ii. Utatuzi wa migogoro kwa njia iliyo rasmi***

Hii ni njia ya utatuzi wa migogoro ya ardhi, inayofuata utaratibu

uliowekwa na sheria mbalimbali za nchi na vyombo maalum vya kuhusika na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Mfumo huu una manufaa kidogo sana kwa mzalishaji mdogo ukilinganisha na ule usiyo rasmi.

Kwa kuwa mfumo huu lazima ufuate sheria za utatuzi wa migogoro ya ardhi ambazo wazalishaji wadogo hawana uelewa nazo sana, pia mfumo huu upo kitaalamu zaidi kiasi cha kumuwia vigumu mzalishaji mdogo kuzifikia haki zake, pia kuna hitajika gharama za uendeshaji mashauri ukiondoa baraza la ardhi la kijiji tu ambalo halina gharama yoyote. Na pia mfumo huu unatumia lugha ambazo wakati mwingine ni vigumu kueleweka kwa mzalishaji mdogo, mfano nyaraka zote kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Mfumo umeelezewa kwa kirefu sana katika kitini hiki, kama utakavyo jisomea hapo chini.

**ANGALIZO:** Ikumbukwe kuwa, katika ngazi ya kijiji kuna usuluhishi wa migogoro ya ardhi unaopitia njia zisizo rasmi mfano wazee wa kimila, Viongozi wa Dini, Wazee Maarufu, au mabaraza ya wazee wa kijiji pamoja na kuwa hawatambuliwi na sheria kuwa ni sehemu ya mamlaka ya utatuzi wa migogoro ya ardhi, bado jamii inaweza kuendelea kutumia mifumo hiyo kwakuwa, ndiyo ipo karibu na jamii zaidi na haina gharama na huchukua muda mchache sana kuifikia maridhiano. Shirika la PELUM Tanzania lingependelea zaidi kuona wazalishaji wadogo wanafikia maridhiano juu ya migogoro ya ardhi kupitia mifumo isiyo ya gharama na isiyotumia muda mwingi kusuluhisha migogoro hiyo ili wananchi waweze kupata muda wa kujihusisha na uzalishaji zaidi kuliko kupoteza muda mwingi katika kutatua migogoro ya ardhi. Kwa wale ambao wangependelea kufuata suluhu za mfumo uliyo rasmi maelezo zaidi ya sheria na vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi vimeelezwa hapa chini.

## 4.0 VYOMBO VYA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

Sheria Ardhi Namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Kijiji Namba 5 zote za mwaka 1999 zinaainisha vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa ambavyo uundwaji wake unaainishwa katika Sheria ya Mabaraza na Mahakama za Ardhi Namba 2 ya mwaka 2002. Mamlaka inayosimamia mabaraza ya ardhi ya vijiji na mabaraza ya kata ni naibu msajili wa vijiji na ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya husika.Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanasimamiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa zinasimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria. Mamlaka zote hizi zina wajibu wa kuandaa makadirio na matumizi ya vyombo wanavyovisimamia kwa mujibu wa sheria.

Sheria ya Mabaraza na Mahakama za Ardhi Namba 2 ya mwaka 2002 inaainisha vyombo vya utatuzi wa migogoro kama ifuatavyo:

### 4.1 BARAZA LA ARDHI LA KIJIJI

***i. Maana na Muundo wa Baraza la Ardhi la Kijiji***

Ni chombo cha usuluhishi wa migogoro ya ardhi ndani ya kijiji kwa kutumia taratibu za mila na desturi za eneo husika. Baraza la Ardhi la Kijiji linaundwa na wajumbe 7 ambao 3 kati yao watakuwa wanawake. Wajumbe hawa watateuliwa na Halmashauri ya Kijiji na kuafikiwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

***ii. Sifa za Wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji***

a. Awe na sifa nzuri na heshima kijijini kama mtu mwenye msimamo na mwenye kufahamu sheria za kimila za ardhi,
b. Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai, pia kwakukosa uaminifu au kukosa maadili.
c. Awe raia wa Tanzania,
d. Awe mkazi mwenyeji wa kijiji,
e. Awe mwenye akili timamu na;
f. Awe aliyetimiza umri wa miaka 18.
g. Asiwe ni mbunge,
h. Asiwe hakimu mwenye mamlaka kwenye Wilaya ambayo ndimo limo baraza,

i. Asiwe mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

Mtu yeyote anayekosa moja ya sifa zilizotajwa hapo juu kwa mujibu wa sheria hawezi kuwa mjumbe wa baraza la ardhi la kijiji.

***iii. Ukomo wa wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji***

Kila mjumbe atatumikia kwa kipindi cha miaka 3 lakini anaweza kuteuliwa tena kwa kuzingatia taratibu zile zile za awali, isipokuwa tu pale ambapo Mjumbe alijiuzulu mapema, kufariki au atakosa sifa tajwa hapo juu.

***iv. Majukumu ya Baraza la Ardhi la Kijiji***

Majukumu ya baraza ni pamoja na kupokea malalamiko yanayohusu ardhi kutoka kwa wanakijiji, kuitisha vikao vya kusikiliza madai ya migogoro kutoka kwa walalamikaji na kusuluhisha migogoro ya ardhi iliyoletwa mbele yake kwa lengo la kufikia maridhiano baina ya wahusika.

***v. Vikao katika Baraza la Ardhi la Kijiji***

Kikao cha baraza kitakuwa na wajumbe 7 hata hivyo kikao kinaweza kufanyika kikiwa na wajumbe wa 4 ambao kati yao 2 lazima wawe wanawake. Baraza litamteua mmoja wa wajumbe kuwa mwenyekiti na mwingine kuwa mtunza kumbukumbu za baraza. Endapo mwenyekiti na mtunza kumbukumbu hawapo wajumbe watakaouhudhuria kikao watamteua mmoja wao kuendesha kikao.

***vi. Mambo ya kuzingatiwa wakati wa suluhu***

Yafuatayo ni Mambo makuu matatu ya kuzingatia wakati wa kutoa suluhu:

a. Kuzingatia misingi yoyote ya mila na desturi za eneo husika.
b. Kuzingatia haki za asili za watu Kama mila na desturi hazitoshelezi.
c. Kuzingatia njia mbadala za utatuzi; kama vile uzoefu wa kutoa suluhu, hekima na busara.

Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, kwa mujibu wa sheria ni vyombo vya kutoa suluhu tu, hayana mamlaka ya kutoa hukumu. Ingawa uzoefu unaonesha vyombo hivi ama kwa kutokujua au kwa kujua vimeku wa

vikitoa hukumu, kutoza faini na kupokea fedha za kufungulia mashauri kutoka kwa wananchi kinyume kabisa na matakwa ya sheria. Vyombo hivi havina budi kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria, hasa kujaribu kutumia zaidi mila na desturi za sehemu husika kwa lengo la kusaidia wazalishaji wadogo kupunguza migogoro ya ardhi na kuvifanya vyombo hivyo kuwa kimbilio la wanyonge.

**ANGALIZO:** Hakuna utaratibu wa kukata rufaa kutoka Baraza la Ardhi la Kijiji kwenda Baraza la Kata kama mwananchi hakuridhia suluhu iliyofikiwa. Kwa maana hiyo mwananchi yeyote ambaye hakuridhia suluhu kijijini basi anaruhusiwa kwenda Baraza la Kata kwenda kufungua shauri Lake. Sheria Namba 5 ya Ardhi ya Kijiji ya 1999 na Sheria ya Mabaraza na Mahakama za Ardhi Namba 2 ya 2002, zinayatambua mabaraza ya ardhi ya vijiji kama vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa njia ya suluhu tu na siyo kutoa hukumu.

## 4.2 BARAZA LA KATA

### *i. Maana na Muundo wa Baraza la Kata*

Mabaraza haya hupokea masuala ya madai, jinai na kuangalia migogoro ya ardhi. Rufaa zake zote za mashauri yanayo husiana na ardhi hupelekwa kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, wakati mashauri mengineyo ya jinai na madai huenda moja kwa moja katika mahakama za mwanzo.

**Muundo wa Baraza la Kata;** Ni chombo cha utatuzi wa mashauri mbalimbali katika ngazi ya Kata kinachoundwa na wajumbe 4 hadi 8 ambapo kati yao wanawake watakuwa 3. Wajumbe wa Baraza huteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata. Baraza la Kata linaundwa na Sheria ya Mabaraza ya Kata Namba 7 mwaka 1985. Hata hivyo katika utatuzi wa migogoro ya ardhi Baraza huongozwa na Sheria ya Mabaraza na Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Namba 2 ya mwaka 2002.

### *ii. Sifa za wajumbe wa Baraza la Kata*

a. Mtu yeyote mkazi wa vijiji vinavyounda kata husika,
b. Awe raia wa Tanzania,
c. Aliyetimiza miaka 18 na mwenye akili timamu.
d. Asiwe mbunge, Diwani, mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji, Baraza la Ardhi la Kijiji,

e. Asiwe mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji au Kamati ya Maendeleo ya Kata,

f. Asiwe mwanasheria au mtu yeyote aliyeajiriwa katika idara ya mahakama,

g. Asiwe mtu aliyewahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai ama utovu wa kukosa uaminifu.

***iii. Kipindi cha ujumbe na Majukumu ya Baraza la Kata***

Kila mjumbe atatumikia Baraza kwa kipindi cha miaka 3 tokea tarehe ya kuchaguliwa kwake na kila mjumbe anaweza kuteuliwa tena kwa kuzingatia taratibu zile zile za awali.Jukumu la msingi la Baraza ni kuleta amani, utulivu na mapatano katika eneo lake kwa mujibu wa Sheria za Ardhi za mwaka 1999 na Sheria ya Mabaraza na Mahakama za Ardhi ya mwaka 2002.

***iv. Uongozi wa Baraza la Kata***

Baraza litaongozwa na Mwenyekiti atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Kata waliochaguliwa. Katibu wa Baraza la Kata atateuliwa na Halmashauri ya Wilaya ambamo Baraza hilo limo baada ya kupata uthibitisho wa Kamati ya Maendeleo ya Kata. Katibu wa Baraza anaruhusiwa kutumikia baraza kwa muda wa miaka Mitano (5) na anaweza kuteuliwa kwa awamu nyingine.

***v. Vikao vya Baraza la Kata***

a. Katika vikao vya usuluhishi vya Baraza lazima liwe na wajumbe 3 na angalau mmoja awe mwanamke.

b. Baraza litaweka kumbukumbu za vikao vyote.

c. Baraza litatakiwa kujitahidi kupata suluhu na linaweza kuahirisha kesi endapo litafikiria kuwa kufanya hivyo suluhu inaweza kupatikana.

***vi. Mambo ya kuzingatia wakati wa Suluhu***

a. Kuzingatia mila na desturi.

b. Kuzingatia haki za asili za watu.

c. Kuzingatia njia mbadala za utatuzi.

***vii. Ukomo wa mamlaka ya Baraza la Kata***

Baraza lina ukomo wa aina mbili katika kufanya kazi zake:

**a.** **Ukomo wa kieneo.** Baraza lina uwezo wa kushughulikia migogoro ya mali au ardhi iliyopo ndani ya kata inayohusika.

**b.** **Ukomo wa kifedha.** Baraza lina uwezo wa kusikiliza na kutoa maamuzi juu ya mgogoro wowote ambao mali au ardhi inayogombaniwa thamani yake haizidi shilingi milioni tatu (3,000,000).

***viii. Uwezo wa kimamlaka wa Baraza la Kata***

**Baraza linaweza kutoa amri za kimahakama kama zifuatazo:**

a. Kuagiza urejeshwaji wa ardhi iliyonyang'anywa.

b. Kumtaka mtu atimize wajibu wake ndani ya mkataba.

c. Kutoa amri au maagizo ya kisheria.

d. Kuagiza ulipaji wa gharama zitakazokuwa zimetumiwa na atakayeshinda kesi au mashahidi wake.

e. Kutoa agizo lolote ambalo litakuwa la haki kwa uamuzi utakaotolewa.

**Ukataji Rufaa kutoka Baraza la Kata**

Upande wowote ambao hautaridhika na maamuzi ya Baraza la Kata unaweza kukata rufaa katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ndani ya siku 45 tangu siku ya kutolewa uamuzi.



## 4.3 BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA

### *i. Maana na Muundo wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya*

Baraza hili ni miongoni mwa vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi Tanzania. Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya huwa linaundwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Ardhi. Kwa mujibu wa sheria, linaweza kuundwa katika ngazi ya Wilaya, Mkoa au Kanda kutegemeana na wingi wa migogoro ya ardhi na nyumba kwenye eneo husika.

**Muundo wa Baraza:**

Baraza hili litaongozwa na Mwenyekiti wa Baraza ambaye kwa mujibu wa Sheria lazima awe Mwanasheria, na atateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya ardhi, na kuapishwa na Mkuu wa Mkoa. Mwenyekiti atashika wadhifa huo kwa muda wa miaka 3 na anaweza kuteuliwa tena baada ya muda huo. Kazi za Mwenyekiti ni pamoja na kusikiliza na kutolea uamuzi migogoro ya ardhi itakayoletwa mbele ya Baraza akishauriana na wajumbe wa Baraza.

Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, kwa mujibu wa Sheria Na.2 ya mwaka 2002 lina wasaidizi wasiozidi saba (7) na watatu (3) kati yao, lazima wawe wanawake. Wasaidizi hawa huteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya ardhi kwa wakati huo kutokana na mapendekezo ya Mkuu wa Mkoa na lazima watoke katika eneo la Wilaya husika.

***Sifa za Wasaidizi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya***

a. Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
b. Mwenye akili timamu,
c. Mkazi wa kudumu wa wilaya husika,
d. Mwenye umri usiopungua miaka 21,
e. Ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai hususani ya kufanya vurugu, kukosa uaminifu au tabia mbaya.
f. Asiwe mbunge, diwani, mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji, mjumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji au Baraza la Kata.

***iii. Ukomo wa mamlaka ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya***

**Baraza lina ukomo wa aina mbili katika kufanya kazi zake**

**a. Ukomo wa Kieneo:** Baraza lina uwezo wa kushugulikia migogoro ya mali au ardhi iliyopo katika wilaya, mkoa au kanda kutegemea mahali baraza limeundwa na kutekeleza shughuli zake kieneo.

**b. Ukomo wa kifedha:** Baraza lina uwezo wa kusikiliza kesi za urejeshaji mali isiyohamishika yenye thamani isiyozidi shilingi milioni Hamisini (50,000,000) na mali inayohamishika isiyozidi thamani ya shilingi milioni Arobaini (40,000,000).

***iv. Majukumu ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya***

Kupokea ushahidi wa ziada kama utakuwa umeletwa, kuangalia kumbukumbu za maamuzi yaliyofanywa na Baraza la Kata, kufanya uchunguzi itakapoonekana ni lazima, kupokea rufaa na kukazia hukumu kutoka Baraza la Kata.

***v. Utaratibu wa usikilizaji wa mashauri***

a. Kesi itaendeshwa kwenye eneo la wazi.

b. Mlalamikaji au mlalamikiwa anaweza kujieleza mwenyewe au kuwakilishwa na wakili au ndugu yeyote au mwanafamilia aliyeteuliwa na mhusika.

c. Baraza litatumia lugha ya Kiswahili au Kiingereza kusikiliza



mashauri kama mwenyekiti atakavyopendekeza, isipokuwa kumbukumbu na hukumu ya mashauri ya Baraza yataandikwa kwa lugha ya Kingereza.

***vi. Uwezo wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya katika rufaa***

Baraza baada ya kusikiliza rufaa linao uwezo wa kuthibitisha, kutengua, kukataa au kurekebisha uamuzi uliotolewa na Baraza la Kata, kufuta shauri lililoamuliwa na Baraza la Kata, kuita na kuchunguza kumbukumbu za mashauri ya Baraza la Kata na kuagiza Baraza la Kata kupitia upya au kurekebisha uamuzi uliofanyika. Pia, baraza litahusika kutoa sababu za kufikia uamuzi huo.

Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya hutekeleza hukumu zake lenyewe kwa kutumia madalali wake. Vilevile Baraza hili linasimamia utekelezaji wa hukumu za Baraza la Kata. Kwa sababu hiyo Baraza la Kata halina mamlaka ya kukaza hukumu zake lenyewe.

***vii. Ukataji Rufaa kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya***

Upande wowote ambao haukubaliani na maamuzi au amri ya baraza unaweza kukata rufaa Mahakama Kuu ndani ya siku sitini (60) toka tarehe ya kusomwa hukumu, ikiwa kesi hiyo ilianzia Baraza la Kata na kwenda Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kama rufani. Endapo shauri hilo lilianzia Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya itabidi rufani ikatwe ndani ya siku 45 kwenda Mahakama Kuu.

## 4.4 MAHAKAMA KUU

Muundo wa Mahakama Kuu; kwa Mujibu wa Ibara ya 108 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inatamka wazi wazi yakuwa kutakuwa na Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo kwa kifupi itaitwa “Mahakama Kuu”. Ibara ya 109 inaelekeza kuwepo kwa majaji ambao ni wateuliwa wa Rais baada ya mashauriano na Tume ya Utumishi ya Mahakama. Majaji husikiliza na kutoa hukumu katika ngazi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.

***i. Usikilizaji wa mashauri***

Mahakama Kuu ina uwezo wa kusikiliza mashauri kwa mara ya kwanza kama ifuatavyo:

a. Mashauri ya madai ya mali isiyohamishika yenye kiwango cha thamani inayozidi shilingi milioni hamsini (50,000,000) na mali inayohamishika inayozidi thamani ya shilingi milioni arobaini (40,000,000).
b. Mashauri yote chini ya Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997, Sheria za Ardhi za mwaka 1999 na Sheria ya Utwaaji wa Ardhi ya mwaka 1967 yanayohusisha serikali.
c. Mashauri yote yanayohusiana na mashirika ya umma.
d. Mashauri yoyote ya ardhi chini ya sheria yoyote iliyoandikwa ambapo mamlaka ya kusikiliza shauri hilo hayakupewa mahakama au baraza lingine.

***ii. Uwezo wa Mahakama Kuu***

Mahakama Kuu ina uwezo wa kuamuru Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kutafuta ushahidi zaidi kukubaliana na maamuzi ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, kubadili na kubatilisha maamuzi ya awali, itakuwa mshauri mkuu wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na ina uwezo wa kukagua kumbukumbu zake wakati wowote na kutoa mwongozo kwa baraza hilo.

***iii. Ukataji rufaa kutoka Mahakama Kuu***

Upande wowote ambao hautaridhishwa na maamuzi ya Mahakama Kuu unaweza kukata rufaa katika Mahakama ya Rufaa ndani ya siku 30 kwa kuzingatia siku 14 za notisi ya kusudio la kukata rufaa. Kila rufaa itakayowasilishwa Mahakama Kuu itasikilizwa chini ya Jaji mmoja, pia rufaa inayohusu masuala ya sheria za kimila Mahakama Kuu ina uwezo wa kuelekeza swala lolote la sheria za kimila kwa mtaalamu au jopo lililoundwa na wataalamu wa mila.

## 4.5 MAHAKAMA YA RUFAA

**Muundo wa Mahakama ya Rufaa:** Mahakama hii inaundwa na Jaji Mkuu ambaye huteuliwa na Raisi kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungo wa Tanzania, Ibara 118 (2). Jaji Mkuu ndiye kiongozi wa Mahakama ya Rufaa na mhimili wa Mahakama za Tanzania kwa ujumla. Katika ngazi hii Rais akishauriana na Jaji Mkuu atateua majaji wa Mahakama ya Rufaa, ambao ni majaji waliotumikia kwa kipindi kisicho pungua miaka kumi na tano (15) katika Mahakama Kuu upande wa Bara na Mahakama Kuu ya Zanzibar.

**Rufaa:** Mtu yeyote ambaye hataridhishwa na maamuzi ya Mahakama Kuu anaruhusiwa kupeleka madai kwenye Mahakama ya Rufaa.
Kwa madai yoyote yanayotoka katika Baraza la Kata yatatakiwa kuambatanishwa na cheti kutoka Mahakama Kuu. Taratibu za uendeshwaji wa mashauri ya rufaa zitaongozwa na sheria na kanuni za Mahakama ya Rufaa.

# 5.0 CHANGAMOTO

**CHANGAMOTO**

Tafiti nyingi zilizofanyika katika Nyanja hii ya vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi zimebaini kuwa mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini unakabiliwa na mapungufu na changamoto mbalimbali na za muda mrefu na zinazotokana na sababu mbalimbali zikiwemo mifumo, masuala ya kiutawala, maadili, uhaba wa rasilimali watu na fedha, na uweledi wa watumishi.

baadhi ya changamoto zilizopo kwa upande wa serikali ni kama za kutelekezwa kwa ardhi, kuhamishwa kwa mifugo, uvamizi wa ardhi ya wafugaji na wakulima, uvamizi wa ardhi ya hifadhi, matatizo ya fidia, utolewaji wa milki ya kiwanja kimoja kwa mtu zaidi ya mmoja, kukua kwa miji, kukosekana kwa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya wawekezaji. na kukosekana kanuni za usimamizi wa uthamini wa ardhi, utatuzi wa changamoto hizi kwa kiasi kikubwa utasaidia kupunguza migogoro katika ardhi.

Kwa upande wa mabaraza ya ardhi ya vijiji; wajumbe wa mabaraza haya wanapata wakati mgumu sana katika utendaji wao, kwa kuwa ni baraza ambalo wajumbe wake hawana uhakika na posho za vikao vyao, kwa kuwa kisheria wao hawaruhusiwi kutoza gharama ya aina yoyote kwa wananchi kwa ajili ya huduma waliyopata. Halmashauri za wilaya na serikali ya kijiji zina mamlaka ya kuendesha mabaraza haya kiuchumi na kiushauri mamlaka hizo zimekuwa hazifanyi hivyo kama sheria inavyowataka. Na hii ndiyo sababu kubwa inayosababisha mabaraza haya yakose wajumbe wa kushiriki katika kuyaendesha, na pia husababisha haya mabaraza kuwatoza wananchi gharama kubwa sana za kuendeshea mashauri ya ardhi.

## 6.0 HITIMISHO

Jitihada kubwa imefanywa na Asasi za Kiraia, kwa kushirikiana na Serikali, katika kujaribu kuelimisha jamii ya kitanzania haki za ardhi kwa mapana yake. Ni ukweli usiopingika kuwa migogoro ya ardhi Tanzania imekuwa changamoto nyingi, kwa kuwa migogoro hii imekuwa ikiongezeka kwa kasi ya ajabu, na kusababisha athari kubwa kwa jamii na taifa kwa ujumla. Kuwa na sheria nzuri na vyombo vingi vya kutatua migogoro ya ardhi haiwezi kuwa dawa pekee na suluhu ya kupunguza au kuondoa migogoro ardhi kabisa. Watanzania wote sasa hatuna budi kuunganisha nguvu kuhakikisha kuwa vyanzo na viashiria vyote vya migogoro vinaepukwa na kuvizuiwa kwa kadri inavyowezekana. Na serikali kwa upande wake kuhakikisha inawajibika katika kuhakikisha utekelezwaji wa sheria za ardhi unakuwa wenye ufanisi zaidi ili kupunguza migogoro ya ardhi isiyo ya lazima.

PELUM Tanzania
S.L.P 390, Morogoro-Tanzania
Simu/Nukushi: +255 23 2613677
Barua pepe: info@pelumtanzania.org
Tovuti: www.pelumtanzania.org